TANGAZO LA SERIKALI Na. 51Cla tarehe 28/1/2025

SHERIA YA KODI YA MAPATO,
(SURA. 332)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya Kifungu cha 10)*

AMRI YA MSAMAHA WA KODI YA ZUIO KWA MALIPO YA PANGO KATIKA MRADI WA UENDELEZAJI WA KONGANI YA VIWANDA KWA KAMPUNI YA SINO TAN KIBAHA INDUSTRIAL PARK YA MWAKA 2025

Jina

**1**. Amri hii itajulikana kama Amri ya Msamaha wa Kodi ya Upangishaji Katika Mradi wa Uendelezaji wa Kongani ya Viwanda kwa Kampuni ya Sino Tan Kibaha Industrial Park ya Mwaka 2025 na itachukuliwa kuwa imeanza kutumika tarehe 26 Agosti, 2024.

Msamaha

**2.** Kodi ya zuio kwa Malipo ya pango katika Mradi wa Uendelezaji wa Kongani ya Viwanda, inayopaswa kulipwa na Kampuni ya Sino Tan Kibaha Industrial Park, imesamehewa.

Ukomo

**3**. Amri hii itafika ukomo wake tarehe 25 Agosti, 2028 na inaweza kuongezewa muda kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa utekelezaji baina ya Kampuni ya Sino Tan Kibaha Industrial Park na Kituo cha Uwekezaji Tanzania kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa tarehe 23 Juni, 2023

Dodoma
31/12/2024

**MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU**
*Waziri wa Fedha*